CHAMA KIKUU CHA USHIRIKA CHA WAKULIMA MKOA WA SINGIDA (SIFACU LTD)

SIFACU LTD
Reg. No. AFF-SGD-SGD-MC-2022-11
Singida, Tanzania
Tel: +255 744 256 768
Website: ……
E-Mail: info@sifacu.or.tz

SINGIDA FARMERS CO-OPERATIVE UNION,
Singida Regional Office,
Bomani, Mughanga, Ward,
P.O Box 123
Singida, Tanzania.

Kumb. Na. SIF/GM/2024/0011 **24 Novemba, 2025**

Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi,
Chama cha Ushirika cha Msingi MTINKO,
S.L.P 35,
MTINKO-SINGIDA.

YAH: UVAMIZI KATIKA ENEO LA USHIRIKA MTINKO.

Tafadhali rejea mada tajwa hapo juu.

2. Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima Mkoa wa Singida (SIFACU LTD) tunafanya kazi kwa kuzingatia Sheria ya Vyama vya Ushirika Nambari 06 ya mwaka 2013 pamoja na Kanuni zake ya mwaka 2015.
3. Mnamo **tarehe 23 Novemba, 2025** Ofisi cha Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Singida kimepokea barua kutoka kwenu isiyo na nambari ya Kumbukumbu inayoelezea uvamizi uliofanyika katika eneo la Ushirika Mtinko.
4. Kwa barua hii, Uongozi wa Chama Kikuu cha Ushirika cha Wakulima Mkoa wa Singida (SIFACU LTD) unapenda kuwafahamisha kuwa baada ya kupata taarifa toka kwenu Ofisi ya Chama Kikuu kilifanikiwa kufanya mazungumzo na Afisa Mtendaji wa Kata ya Mtinko ili kujua uhalisia wa jambo hilo na kisha kufikia makubaliano yafuatayo:
    i. Zoezi la uendelezaji linalofanyika katika eneo la Ushirika Mtinko lisimame kwanza hadi utakapopatikana ufumbuzi wa hiyo sintofahamu.
    ii. Kwa kuwa kutafuta wadau wa maendeleo katika eneo husika kwa manufaa ya wakulima ni moja ya jukumu la Ushirika, Mdau anayehitaji kufanya kazi katika maeneo ya Ushirika anapaswa kuwasiliana na Wanaushirika ili kuona namna bora ya kunufaika na uwepo wake mdau, hivyo lazima Mtinko AMCOS ashirikishwe na kuridhia uendelezaji huo katika eneo la Ushirika kwa niaba ya Ushirika Mkoa wa Singida.

iii. Kutokana na kuwa tayari Mtinko AMCOS tayari wamepitisha bajeti yao katika ngazi ya Mkoa kwa ajili ya uendelezaji, ni vyema kufuata utaratibu wa kiushirika kuondoka mgogoro.

5. Kwa barua hii mnaelekezwa kuwa na utulivu kwa kipindi hiki ambacho tunaoendelea kutafuta ufumbuzi wa suala hili kwa kushirikiana na Ofisi ya Afisa Mtendaji Kata ya Mtinko pamoja na mamlaka nyingine za Serikali toka ngazi ya Mkoa.

6. Bodi ya Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Singida (SIFACU LTD) inaendelea kuwashukuru kwa ushirikiano inaoendelea kuupata kutoka kwenu. Bodi ya Uongozi ipo tayari kuendelea kushirikiana katika kuwahudumia Wakulima wa Mtinko na Mkoa wa Singida kwa ujumla.

Pamoja na salamu za Ushirika Bodi ya Chama Kikuu SIFACU LTD inawatakia utekelezaji mwema wa majukumu yenu ya kila siku.

Wako katika Ushirika,

……..
NOEL ANANIA ELIA
MENEJA MKUU-SIFACU LTD

Nakala:
Katibu Tawala (M),
Mkoa wa Singida,
S.L.P 5,
SINGIDA

Mwenyekiti wa Tume ya kufuatilia mali za Ushirika (M),
Mkoa wa Singida,
S.L.P 123,
SINGIDA.

Mwenyekiti wa Bodi,
Chama Kikuu cha Ushirika Mkoa wa Singida-SIFACU,
S.L.P 123,
SINGIDA.

Ndani ya jarada

Afisa Mtendaji,
Kata ya Mtinko,
S.L.P
MTINKO.

Ndugu Yessaya Mande,
Mjumbe wa Tume,
Tume ya kufuatilia mali za Ushirika (M)
S.L.P 123,
SINGIDA.